**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**15 Agosti 2009**

**Waliohudhuria**
Rahma Ali
Juma Ali Salehe Jongo
Abdul H Mwaibambe
Mohammed Samwely
Shamte J Kisoma
Filbert Mbecha
Jumanne Ayuba
Elaine Baker-Guni
Beda John Mkusu
Muharami Amir
Amos Sindano
Mejah Mbuya
Dominata Rwechungura
Husein Hamza Hamisi
Saidi Brashi
Ramadhani Rajabu Nyengo
Idrisa Kessi Zongo
Ally Athuman Jumbe
Edgar R Paulo
Paulo Atibu Hatibu

**Msafara**
Tulipata jibu kwa email kutoka Zantel na Ubalozi wa Ireland kusema kwamba hawawezi kutupa udhamini. Tumepata jibu kwa sanduka la posta kutoka kwa Ubalozi wa Uholonzi na Japan kusema kwamba hawawezi kutupa udhamini.

Ubalozi wa UK (British High Commission) walisema kwamba wanatoa udhamini kwa ajili ya miradi yanayohusika mabadaliko ya majira. Basi tukiandika upya proposal kwa kuongea zaidi kuhusu mabadaliko ya majira kuna uwezekano kupata udhamini. Elaine ataandika upya.

Elaine ataleta nakala zaidi za proposal na barua za China, Denmark na Sweden ili tufuatalie.

**Mradi wa Wamba**
Tuliwasiliana na mkuu wa shule ya Mbondole na tumekubaliana tufundishe alhamisi na ijumaa tarehe 27 na 28 agosti. Alisema watakuwa na wanafunzi 65. Mejah alisema kuna uwezekana wa kupata reflecta jaketi bure – atapata taarifa zaidi. Tunabaki na jaketi 34, helmet 35 na mwongozo 37 basi kuna haja ya kuongeza 30 30 ili tuwe na za ziada.

Tulichagua waalimu: Juma, Filbert, Hussein Hamza, Mohammed, Paulo. Filbert atashughulika na kununua helmet na jaketi zaidi.

**Kutafuta mikutano**
Juma alipeleka kwa serikali ya mtaa.  Filbert alipeleka kwa Waziri wa Miundombinu (aliacha kwa katibu wa waziri) na nakala ya barua ya meya kwa diwani Lupilya.  Saidi alipeleka kwa Komanda Kombe na ofisi ya Meya. Tulipata jibu kutoka kwa Komanda Kombe – anakubali kutana nasi na sisi tuchague tarehe.  Tulichagua jumanne tarehe 25 mwezi wa nane saa nne asubuhi.  Elaine ataandika barua kupendekeza tarehe hiyo na pia kuwaalika traffic police kwenye mafunzo ya Mbondole.

Kwenye mkutano tutaleta picha za magari yanapaki kwenye service roads na tutaomba traffic police watangaze rasmi kwamba kupaki kwenye service roads hairuhisiwi na pia tutaongea kuhusu kushirikiana katika mafunzo ya usalama wa baisikeli.

Pia siku ile tarehe 25 Edgar atatupatia mkutano na ndugu wake anayefanya kazi UNDP.

**Uchaguzi wa 2010**
Paulo alipeleka barua CCM, TLP, CUF, CHADEMA na NCCR-Maguezi.  Mpaka sasa tumepata jibu kutoka kwa CUF tu.  Wanasema wanatukaribisha kuandika maoni yetu kwanza halafu baadaye tunaweza kutana nao.  Mejah ataandika barua yenye maoni na tutapitisha wiki ijayo.  Elaine ataleta nakala zaidi za barua ili tufuatalie jibu.

**Marekebisho madogo madogo ya barabara**
Kwenye mkutano wa wiki jana wanachama walipitia fomu ya kutoa repoti ya matatizo barabarani na wamekubali nayo.  Elaine ataleta nakala nyingi ili tuwenazo ofisini.

**Mwaliko kwenye wiki ya mabadliko ya majira**
Tulipata mawasiliana kwa email kutoka kwa shirika linaloitwa EWAT – Environmental Watch Association of Tanzania – mwenyekiti ni Deodatus Kiriba.  Wanaandaa wiki kuhusu mabadaliko ya majira huko Sokoine University of Agriculture, Morogoro tarehe 20-26 Septemba 2009 na wametualika.  Wiki hii inaungaisha na kampeni ya dunia ya "Seal the Deal" ambayo inaita serikali za dunia wakubaliana kuhusu suala hili kwenye mkutano huku Copenhagan, Denmark mwezi wa desemba.  Pia EWAT watapenda kushirikiana nasi kwenye msafara wa baisikeli.  Tunawasiliana nao kuhusu vipi kushirikiana zaidi.

**Shirika la Fasta Cycle Couriers**
Bwana Bukuku, ofisa wa wilaya ya shirika, alisema atahudhuria mkutano wa leo lakini bada ya hapo alituma message kusema atakuja wiki ijayo.

**Watu wa I-CE kututembelea**
Mejah alitangaza kwamba watu wa I-CE watakuwepo Tanzania na watatutembelea UWABA tarehe 31 agosti mpaka tarehe 5 septemba.  Wanapenda kuongea kuhusu vipi kuanzisha mradi wa kutoa mikopo kwa ajili ya kununua baisikeli.

**Re-cycle**
Elaine ataprint nakala nyingine ya katiba ili Mejah afuatalie namba ya TIN.

**Wimbo**
Mejah bado hajatengeneza CD cover kwa wimbo.

**Mafunzo ya Lugha**
Wiki tatu iliyopita mafunzo yamesimamishwa kwa sababu Juma alifunga ofisi akaondoka bila taarifa.  Wiki jana mwalimu alikuwa na umwa.  Tulipendekeza kwamba mwalimu aje kwenye mkutano wiki ijayo ili tuongee.  Abdul atawasiliana naye.

**Ufunguo wa ofisi**
Filbert atanunua kufuri na funguo tatu mpya kwa ajili ya ofisi.

**Website**
Elaine alilipa UCC kwa ajili ya kuhost website mpya kwa mwaka moja.  Kulikuwa na shida ya kusajili anwani ya www.uwaba.or.tz kwa sababu imeshasajiliwa na rafiki wa Mejah (Jones) ili kutusaidia – kwa sasa tunawasiliana naye ili kuhamisha usajili kwa UCC.

**Tutafsiri "Turning Point"**
Mejah ataangalia DVD ya "Turning Point" na atatafuta jinsi ya kutafsiri au kuweka subtitles.

**Repoti za mikutano**
Mejah alisoma repoti kuhusu mkutano wa usalama barabarani, ubelgiji.  Elaine atachapa repoti Dominata aliyoandika kuhusu mkutano wa Tanga.

**Mambo mengine**
Wanachama wengine walipendekeza tubadlishe katiba ili tushughulike na nchi nzima na siyo Dar es Salaam tu.  Elaine alisema itakuwa ngumu kwa sababu lazima kupata 75% ya wanachama (ambao ni zaidi ya 200) kuhudhuria mkutano na pia lazima kubadilisha cheti cha usajili serikalini.  Lakini tunaweza kusaidia wapanda baisikeli kwenye miji mengine kuanzisha NGOs zingine za baisikeli huko.

**Hela na guta**
Dereva wa guta (Ramadhani) alilipa Tsh 25,000 na sasa hana deni.

Mejah alimpa Filbert Tsh 10,000 na sasa bado anadaiwa Tsh 77,000 (mikopo ya Nairobi na Ubelgiji).

Elaine alitumia Tsh 130,850 ya hela ya UWABA pamoja na Tsh 11,150 ya hela yake kulipa ada ya website kwa mwaka (Tsh 142,000).  Alirudishiwa Tsh 10,000 na Tsh 1,150 anachangia.

Dominata alirudishiwa Tsh 13,000 ambayo alitumia kununua helmet na jaketi ya reflecta kwa meya wa Tanga.
Sasa Filbert anabaki ya hela ya UWABA Tsh 12,000.  Atatumia baadhi ya hela kununua kufuri ya ofisi.

Guta inataka mpira mpya.  Bei ya mpira ya ubora ni Tsh 28,500 – Tsh 30,000.  Mejah atampa hela kwa Filbert na itakatwa kutoka deni yake.

**Uchaguzi wa kamati**

Tulikubali kuwa na uchaguzi wa kamati wiki ijayo.  Elaine atatuma SMS kwa wanachama ili wawe na taarifa.